

## SAUTI YA DHIKI: HAZINA YA KUHIFADHI, KUKABILI NA KUFUATILIA MAOVU YOTE KWA NJIA YA AMANI

Nahashon A. Nyangeri na Hassan R. Hassan

### Ikisiri

*Kenya imepitia kipindi kisicho mfano cha kukiukwa kwa haki za binadamu. Hili limedhihirika kupitia migogoro na mizozo ya mara kwa mara ya kikabila. Ukiukwaji huu unajumuisha mauaji ya halaiki, mateso, uovu, pamoja na uhalifu wa aina mbalimbali. Kwa kuzingatia ukweli huu, wasanii, wakiwemo washairi, pia wanajitokeza kuchangia katika suala hili. Kwa kutumia diwani ya Sauti ya Dhiki (Abdalla, 1973), makala hii inatalii jinsi dhuluma na kususia huwasilishwa kishairi. Ushairi wa Kiswahili unajitokeza kama chombo cha kuangazia dhuluma mbalimbali za kijamii na za kisiasa na kama njia ya kuelezea hisia za kibinafsi kuhusu dhuluma. Ushairi unasomwa kama njia ya kuwawezesha watu kuasi na kupinga hali na mifumo inayowakandamiza, kuwasilishia yasiyowasilishika, na kutoa sauti mbadala ya kuelezea masuala yanayoisa kama jamii.*

### Lugha na Sanaa ya Kusema “La! kwa Ukatili”

Historia ya Kenya imejaa visa vya mauaji ya kutisha ambayo baadhi yake yanasemekana kuwa yalifadhiliwa na vyombo vya usalama kwa kisingizio cha oparesheni ya usalama. Kwa mujibu wa Ripoti ya Tume ya Haki na Maridhiano, utawala wa serikali mbalimbali umechukuliwa kuwa mwendelezo wa ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu (TJRC, 2013). Ukiukaji huu umejitokeza kupitia vita<sup>3</sup>, mauaji<sup>4</sup>, mateso<sup>5</sup>, adhabu ya pamoja, kumnyima mtu mahitaji ya msingi, mauaji ya kisiasa,<sup>6</sup> kutia mtu kizuizini, dhuluma pamoja na unyanyasaji wa wapinzani wa kisiasa na wanaharakati wa haki za binadamu. Orodha hii ndefu ya visa vya ukatili imevuta makini ya washairi ambao wana jukumu la kuwa sauti ya mnyonge. Uchunguzi wa tungo za fasihi ya Kiswahili unaonyesha matukio ambapo Waswahili walitumia sanaa zao kudai uhuru wao wa kisiasa na wa kiuchumi. Ushairi ulijitokeza kama njia ambayo kwayo msanii aliwapatia sauti ‘wanaoteswa’ (Dawes, 2007). Makala hii inafafanua jinsi suala hili la ukatili lilivyoangaziwa katika *Sauti ya Dhiki*. Diwani hii ilitungwa na Abdilatif Abdalla baada ya ukoloni nchini Kenya. Ingawa hii ni diwani ya mwandishi mmoja tu, ina data za kutosha

---

<sup>3</sup> Mifano ni pamoja na vita vya Maumau na vya Mashifta.

<sup>4</sup> Haya ni pamoja na mauaji ya Kedong, Ususiaji wa Giriama, Mauaji ya Kollowa, ya Lari, ya Hola, ya Turbi na ya Bubisa (2005), ya Murkutwa (2001), ya Loteteleit (1988), ya Bulla Karatasi (1980), ya Wagalla, (1984), ya Lotirir (1984) ya Malka Mari (1981), na ya Garissa (1980).

<sup>5</sup> Hasa vyumba katika majengo ya Nyayo na Nyati vilivyotumiwa kuwatesa wapinzani.

<sup>6</sup> Waliouawa ni pamoja na Pio Gama Pinto, Tom Mboya, J.M. Kariuki, Dr. Robert Ouko, Askofu Alexander Muge Crispine Odhiambo Mbai, na Padri John Kaiser.

kutoa mwanga kuhusu ukatili nchini Kenya, ikitambuliwa kwamba naye alikuwa mmoja wa waathiriwa wa ukatili. Uchanganuzi huu unaegemea matukio ya kihistoria ambayo yametumika kudhihirisha ujumbe unaowasilishwa katika kazi hii.

Abdilatif Abdalla aliandika *Sauti ya Dhiki* wakati akitumikia kifungo chake katika Gereza la Shimo la Tewa nchini Kenya. Diwani hii inaweka wazi ukatili aliopitia kizuizini, mahali ambamo ‘wahalifu na wanaharakati wa kisiasa wanahudumu pamoja’ (Povey, 1993:99). *Sauti ya Dhiki* humchochea msomaji kujiuliza kama Dawes "Ni nani ana haki ya kusema?" na "mipaka ya haki hiyo ni ipi?" (Dawes, 2007:4). Neno lililoandikwa limekuwa kama taa gizani ili kushuhudia maovu hayo. Kauli za ukatili na dhuluma walizopitia wahusika mbalimbali zinatoa majibu kwa swali "ina maana gani kuwa Mkenya?" *Sauti ya Dhiki* ni mfano kabambe wa kazi hizo. Kazi hii ni kumbukumbu muhimu kuhusu matukio ya kipindi hicho cha mateso na dhuluma, ingawa zipo nyingine kadhaa kama *Chembe cha Moyo* ya Alamin Mazrui, *Kichomi* ya Euphrase Kezilahabi, na *Bara Jingine* ya Kithaka wa Mberia. Uteuzi wa diwani hii umechochewa na ukweli kwamba mtunzi alikuwa mmoja wa waathiriwa wa dhuluma, hivyo anatoa mtazamo wa ndani kuhusu suala hili. Azimio la mtunzi ni kutafuta haki na kuhakikisha kuwa sauti kwa waliodhulumiwa katika jamii inakuwa imara.

Kulingana na Adorno, "maumivu yana nguvu ya kuibua furaha kutoka kwayo." Maumivu yenyewe wanayoyapitia wanaodhulumiwa huwafanya kupindua "hali isiyofikirika inaonekana kuwa na maana fulani, inabadilishwa; kitu cha hofu yake huondolewa" (Dawes, 2007:8). Kwa mantiki hii, watunzi waliowaathiriwa wa dhuluma huyaangazia machungu waliyoyapitia kizuizini kwa kutumia lugha fiche ya kuwawezesha kuyawasilisha machungu wanayoyapitia. Hutumia lugha batini kama nyenzo ya kuwasilisha ujumbe wa haja ya kujikomboa kwa jamii. Jambo hili tunaliona katika sanaa inayotumia lugha ya Kiswahili kwa jumla, hasa ushairi wake. Waliopigania ukombozi kutoka kwa utawala wa kikoloni walitumia lugha ya Kiswahili kwa njia mbili; hivyo kuliibuka lugha yenye maana mbili: maana moja inayolengwa kwa wakandamizaji ambao wangeweza kuelewa tu maana ya nje, na maana ya ndani ilikuwa kwa wale waliokandamizwa. Maana ya ndani ilikuwa tata na ngeni kwa wakandamizaji kuielewa. Utata huu ulisitiriwa katika vazi la ushairi ili uvuke vizingiti vya kukaguliwa na kutupiliwa mbali na waliofumbwa. Kisanaa, fasiri hizi ni vidokezo vya kufafanulia maana batini ambazo haziwezi kufanywa moja kwa moja kutokana na ukweli kuwa, mara nyingi, ushairi hutegemea iktisadi ya maneno kuuwasilisha ujumbe wake. Hii ni mojawapo ya sifa aula iliyo katika kiini cha lugha ya kisanaa, ukiwemo ushairi. Ushairi hutumiwa kama chombo cha kiufundi kwa sanaa ya usemaji kuelezea na kuweka bayana mitazamo, maoni na misimamo. Utata, upungufu na uzito wa lugha ya kishairi huwezesha kutoa maoni

nyeti kuhusu masuala ya kijamii. Sehemu inayofuata inachanganua jinsi mtunzi wa *Sauti ya Dhiki* alivyochota sifa hizi kuwasilisha ujumbe wake ambao vinginevyo usingewasilishwa nchini Kenya nyakati hizo.

Zipo tafiti kadhaa ambazo zimeangazia suala la vita na machafuko nchini Kenya (kwa mfano, Karari, 2014). Baadhi ya tafiti zimependekeza kususia kama suluhisho la kuyamaliza machafuko nchini Kenya (kwa mfano Wambura, 2008; Katho, 2013). Hata hivyo, changamoto kuu imekuwa jinsi ya kufanya hivyo bila kuhusisha vita, makabiliano, mapambano na umwagikaji wa damu. Mapendelezo ya uchunguzi wa Karari ni kurekebisha kwa asasi ya uongozi, ingawa anahofia uwezekano wa hilo pasi na umwagikaji wa damu kama anavyosema: “Haki kwa raia wa Kenya haiwezi kupatikana kwa njia ya amani au ushawishi, bali kupitia kujitolea na kushurutisha (Karari, 2014:298).”

Ikikumbukwa kwamba serikali ina mamlaka ya kukomesha juhudi hizo, matumizi ya lugha huwa muhimu. Hii ni kwa sababu, wakati wa mabadiliko ya mfumo bado hayajawadia. Linalohitajika ni kukuza na kujenga majukuwaa ambayo yanaweza kukitwa na kuendelezwa. Hili tunaamini kwamba linajitokeza katika uwanja wa sanaa.

### **Liwe liwalo, nitasema: Heri vina kuliko vita**

Kwa kawaida, mnyonge anaponyanyaswa hutafuta njia ya kujikomboa. Mara nyingi wengi huishia kumkabili anayedhulumu katika vita. Hata hivyo, mara nyingi madhara ya mbinu ya kutumia vita huwa mabaya zaidi kuliko ilivyokusudiwa. Kwa sababu hii, kutumia lugha kujadiliana ili kusuluhisha mizozo na udhalimu ndiyo njia ya pekee inayoweza kumhakikishia anayedhulumiwa suluhisho la kudumu. Hata hivyo, kudhibitiwa kwa mawasiliano ya wanaodhulumiwa kunakotekelezwa na utawala huchochea wanaodhulumiwa kuufumba ujumbe wao kwa namna ambayo inawezesha kuvuka kizingiti cha ukaguzi na udhibiti. Hapa ndipo ushairi unajitokeza kama nyenzo mwafaka ya kusambaza ujumbe wa dhuluma wanazozipitia wengi wanaodhulumiwa, pasi wanaowadhulumu kutambua hilo kwa wepesi.

Baada ya kutambua kwamba sharti anayedhulumiwa kuamua kuwa na msimamo thabiti katika kuchukua hatua ya kujitetea, mtunzi wa *Sauti ya Dhiki* anaamua kuupitisha ujumbe huu kishairi. Kushikilia msimamo ndiyo njia ya pekee ya kuhakikisha dhuluma na maovu yamekomesha. Katika shairi la "N'shishiyelo ni Lilo" (kur. 1-4) mshairi anaapa hadharani kwamba hatakoma kuyakemea matendo ya kikatili wanayofanyiwa wanaopinga serikali na viongozi. Anafahamu kuwa wapinzani watateswa na kutendewa unyama wa kila aina kama ilivyoonyeshwa katika ubeti wa nne na wa tano:

Kweli imenitongeya, kwa kuinena mwendani  
Wale nalowaambiya, wamenitiya dhikini  
Wameniona mbaya, kumshinda Firauni  
Kweli, sasa naamini, si wangi wapendao

Kweli naliwaambiya, wakuu wa nti hini  
Haeleza moya moya, kwa wanati wa ntini  
Kuhusu walofanyiya, upande wa Upinzani  
Sasa kuwamo tabuni, nalipwa kwa hiyo kweli

Maelezo hayo kuhusu alivyoteswa yanatuelekeza kusema kwamba kazi hii ya *Sauti ya Dhiki* ni tawasifu au ushuhuda wa mwathiriwa kuhusu dhiki na mateso wanayofanyiwa wanyonge. Ujumbe huu huu wa kuteswa kwa wapinzani unaendelezwa katika shairi la "Kamliwaze" (uk. 5). Ili kuuendeleza na kusisitiza ujumbe "Kamliwaze", mwezi mmoja baadaye anaandika "Tuza Moyo" (uk. 6). Huu ni ubeti mmoja tu lakini uliobebeshwa ujumbe mzito unaohusu kumtia moyo na kumhimiza. Katika ubeti huu, mshairi anaeleza kile kinachohitajika katika juhudi za kupambana na dhuluma anazozipitia. Anataja uvumilivu na maombi. Anaeleza kuwa haya ndiyo yanafaa kuwapo ili kuhakikisha kwamba mateso yote yamekwisha.

Haya ndiyo maudhui yanayotawala utunzi na kuwafanya malenga wa ushairi wa Kiswahili kuwa makuli wa matumaini kama inayodhihirika katika shairi "Yatakoma" (uk. 28). Katika shairi hili, mshairi anasisitiza kuwa, wakati wa mateso, jambo muhimu ni uvumilivu kwa wote, mtunzi mwenyewe akiwa mmoja wao. Hili linadhihirika pale anapoihimiza "nafsi yake" iwe na uvumilivu (ubeti 2) kwa kuwa lililo muhimu ni tuzo atakayopokea mwishowe (ubeti 6). Anasema:

Utuwe mtima, na kutabaradi  
`Papatuwe kama, uwa la waridi  
Zitakapokoma, zakwe tashididi

`Talivaa koja, la yangu subira  
Nipate natija, ilo barabara  
Subira kwa mja, ndilo jambo bora

Kwa hakika, "maumivu katika sura zake zote si chochote isipokuwa kuvunja na kuvurugika kwa nafsi ya mtu" (Boushaba, 1988:63). Katika hali hii lililo bora ni uvumilivu wala si kushiriki vita kwa kuwa vitaishia kuleta maangamizi makubwa zaidi.

Tunaweza kutumia lugha ili kubadilisha shughuli za vurugu na mateso kwa namna ambayo itakuwa na matokeo makubwa zaidi kuliko vile mapambano ya risasi yanavyoweza kufanya. Hii ni wazi kwa kuwa ushairi hupania kuondoa maumivu ya

kimwili kwa kutumia maneno yanayowawezesha wasanii kutenda aina fulani za vitendo usemi. Risasi ya ushairi hulengwa kwenye ngome ya nafsi na kumhakikishia mtu uhuru kamili ambao utamchochea kuchukua hatua ya kuyamaliza mateso na ukatili. Kwa namna hii, ushairi hugusia suala hili tata kwa kuwasilisha suluhisho kwa busara badala ya matumizi ya nguvu kupitia mtutu wa bunduki; yaani, kutumia usanii badala ya mabavu. Mtunzi anajitahidi kuifikia nafsi ya msomaji badala ya kutaja tatizo kwa jumla. Hii inalenga kuwasukuma wasomaji kuchukua hatua fulani. Swala hili la mtu kuzungumza na nafsi yake huwa na umuhimu mkubwa. Kipengele hiki kinaongezwa kama mojawapo ya yale yanayohitajika katika kukomesha dhuluma, mateso na vurugu. Mazungumzo haya na nafsi yamejitokeza katika shairi la "Moyo Iwa na Subira" (kur. 48-50). Katika ubeti wa sita mtunzi anataja sababu ya kuushawishi moyo wake ukome kulia:

Utajiumiza mbavu, kulia usiposita  
Utashikwa na chechevu, na homa utaipata  
Upate na maumivu, langu usipofuwata  
Nyamaa matozi futa, zidi kuwa na subira

Mshairi anaueleza moyo wake kwamba, kwa kawaida, dunia imejaa uovu; kwa hiyo kuomboleza hakusaidii kwa vyovyote vile. Wakati wowote ule, hayo hayatakuwa mateso machungu ya mwisho; mengine zaidi yamo njiani. Mtu anapaswa kujiandaa kuyakabili. Kile kinachohitajika ni uvumilivu kwa sababu mabadiliko hayaepukiki. Kwa hiyo, mshairi anampa kila mmoja changamoto ya kuzungumza na "nafsi" yake kama njia ya kujiandaa kukabili tukio lolote linaloweza kutokea kama askari walio tayari kupambana na kila aina ya uovu.

Jambo hili linamfanya mshairi kuwa wakili wa hekima na uvumilivu kama alivyo Voltaire (Treasure, 1985:156). Mishororo hii ya kinabii iliishia kutimia kupitia vita mbalimbali, mauaji, na mateso kwenye vituo vya polisi. Hatimaye, ilifikia kilele chake katika vita vya baada ya uchaguzi wa 2007/2008 nchini Kenya. Kwa hiyo, tofauti na wanahistoria, washairi "hawawasilishi kilichotokea, bali kinachoweza kutokea" (Bressler, 2007:23). Kwa mkondo huu huu, Abdilatif Abdalla katika *Sauti ya Dhiki* anaandika kinachoweza kutokea, jambo linalothibitisha kuwa ushairi wa Kiswahili unaelekea kuwa wa kifalsafa na wa tukio mahususi badala ya kuwa wa kihistoria na unaoelezea maswala ya kilimwengu kwa jumla. Anawasilisha katika jamii kama inavyopaswa kuwa wala si jinsi ilivyo. Jaribio lake la kujenga maadili na busara kwa kutumia ucheshi limefaa (Bressler, 2007:33). Abdalla anaweza kurejelewa kama mmoja wa malenga "adhimu" wa ushairi wa Kiswahili.

### **Vichocho na Suluhisho kwa Dhuluma Zisizokoma**

Dhuluma zina historia ndefu nchini Kenya, zikijitokeza hata enzi za kabla ya uhuru (TJRC, 2013). Dhuluma hizi huchochewa na tofauti za kijamii, kisiasa na kiuchumi. Kutokana na athari za dhuluma hizi kwa watu binafsi na jamii kwa jumla, pana haja ya kuangazia sababu pamoja na kupendekeza mbinu za kuzikomesha ili kuhakikisha kuna usawa na amani katika jamii. Sehemu hii inachunguza jinsi suala hili linavyojitokeza katika *Sauti ya Dhiki*.

Kupitia jazanda ya jipu, Abdalla katika shairi la "Jipu" (kur. 7-8) anasimulia jinsi dhuluma zianzavyo kwa njia sahili na isiyoweza kushukiwa kuwa itabadilika baadaye na kukomaa na kuwa ukatili mkubwa wa kila aina ya haki za binadamu. Anajutia kutotambua hili kwa wakati ili aweze kuchukua hatua zinazofaa kuzuia haya kutokea. Kwa kuwa sasa amechelewa, kimbilio lake la pekee ni wakati. Hata hivyo, ili haya yaweze kutokea, lazima ajiunge katika vita vya kulitibu jipu kama asemavyo katika ubeti wa tisa kuwa:

ˆTaliminya litumbuke, lisinisumbuwe tena  
Usaha wote utoke, utoke nikiuona  
Midamu itiririke, kama ng’ombe alonona  
Jipu hili mwana lana, M’ngu mbwalipa hizaya

Kisha anajitolea kutoa dawa yake ya kishairi kwa ajili ya kurejesha afya yake. Anasema kwamba jipu litapona pale madhalimu watakapokuwa wameshindwa (ubeti 11):

Baada ya yote haya, jaraha niliuguze  
Kwa madawa kulitiya, ili kwamba yalipoze  
Irudi yangu afiya, na zaidi niuguze  
Nirukeruke niteze, kwa furaha kuningiya

Siri ya kukomesha dhuluma, vurugu, mateso na ukatili nchini imo kwa waathiriwa wenyewe. Wanahitajika kutambua hali inayowakabili kisha wakajitolea kuchukua hatua. Mwito wa Abdalla kuhusu umuhimu wa uvumilivu na kujitoa kudai haki, badala ya kulalamikia hali ya sasa unajitokeza tena katika shairi la “Mamba” (uk. 10). Kupitia hali ya kutodumu kwa binadamu, mtunzi anawapa matumaini wanaodhulumiwa kwamba wajipe moyo kwa kuwa si muda mrefu, mtesi wao ataondoka. Katika ubeti wa mwisho wa shairi hili mtunzi anaweka wazi kuwa mamba hataishi milele. Anaeleza:

Afahamu, mtu hajui la kesho  
Hatadumu, angatumiya vitisho  
Maadamu, lenye mwanzo lina mwisho

Hii ni kinyume na jinsi mamba mwenyewe anavyodhania kama ilivyofafanuliwa katika ubeti wa pili. Katika ubeti huu, mamba anajigamba na kujinadi kuwa yeye ni kiumbe hodari atakayeishi milele. Anajinadi na kujisifu kwa sifa ambazo zimewatia wengi ari ya kuwatendea wenzao maovu na ukatili. Kwa sababu ya uovu wake na nguvu za uharibifu, mamba huashiria ghadhabu, ubaya na ukatili (Cirlot, 2001:67) pamoja na unafiki wa binadamu (Ferber, 2007:47-48). Hizi ndizo sifa za vyombo vya dola vinavyoendeleza ukatili na unyama kwa Wakenya wasio na hatia, kama Abdilatif Abdalla aliyefungwa jela kwa kuisuta serikali katika chapisho lake maarufu la "Kenya Twendapi?" Katika chapisho hilo, mshairi alikuwa akiwarejelea wanasiasa kama mamba aliye mwingi wa ukatili dhidi ya binadamu (Chacha, 1992).

Kama nyongeza kwa shairi la "Mamba", wakati akiwa gerezani, aliandika ngonjera ya "Mnazi: Vuta N'kuvute" (uk. 17-22). Katika beti namba 4-7 za shairi hili, anataja kuwa chanzo cha ugomvi ni kubinafsisha rasilimali za umma. Alii anapodai kwamba Badi ashuke kutoka juu ya mnazi ili naye pia aukwee kupata mgao wake, anatumia na baadaye kupokonywa sehemu yake ya umiliki wao wa pamoja wa mnazi huo. Hii ndiyo hali iliyojitokeza katika Kenya huru wakati makamu wa Rais wa kwanza Jaramogi Oginga Odinga alipotengana na Rais Jomo Kenyatta mwaka wa 1967. Makamu huyo wa Rais baada ya kutengana na Rais aliunda chama chake cha kisiasa kilichoitwa KAU. Vuta N'kuvute iliyofuatia baina ya viongozi hawa wawili ilichochea maandamano na vurugu zilizoishia katika mauaji ya watu wengi jijini Kisumu mwaka 1969 wakati wa ufunguzi wa Hospitali ya Russia, ambayo kwa sasa inajulikana kama Jaramogi Oginga Odinga Teaching and Referral Hospital. Inasikitisha kwamba, wakati wa uhuru, KADU, kilichokuwa chama cha wachache, kilijiunga na KANU. Hili linasawiriwa Abdalla katika shairi hili pale Badi na Alii walivyongana; hata hivyo, punde tu wanatambua kwamba urafiki wao ulikuwa pambo na umoja wao kuwa wa muda mfupi. Katika majibizano yao, mshairi anataja kuwa dawa mujarabu ni mazungumzo ya uaminifu kinyume na msimamo mkali anaouchukua Badi. Kiburi, majigambo na ujuba huvuvia machafuko zaidi; hivyo, Alii anaapa kudai mgao wake. Haya yanaishia katika maovu, ukatili na udhalimu uliotajwa hapa awali. Majibizano marefu kati ya Alii na Badi yanathibitisha madai yaliyotolewa katika TJRC Juz. 2A kwamba "mara nyingi, mauaji hayo ni zao la mivutano ya muda mrefu na hisivu ya kijamii na kiuchumi" (TJRC, 2013:155).

Kwa mtazamo wa dayolojia ya Ki-Bakhtini, kupitia wazo la heteroglosia na uhulutishi, Alii na Badi wanawakilisha mazungumzo ya ndani ya mtu na "nafsi" yake ambapo kuna "sauti" kadhaa zilizo muhimu kwetu. Hoja hii ina maana sawa na ile ya Treasure (1985:156) kuwa kuna "vita vya wenyewe kwa wenyewe katika kila nafsi". Katiba ya UNESCO inatambua kuwa vita huanzia katika akili za wanadamu,

hivyo ni katika akili hizi za wanadamu ambako lazima tujenge ngome ya kuitetea amani (UNESCO, 2002:7). Katika aina hii ya vita vya wenyewe kwa wenyewe, sauti inayoshinda katika mjadala huu ndiyo inayoufafanua ufahamu wetu. Kwa namna hii, mshairi humpa msomaji jukumu la kuchagua kusitisha au kutositisha vitendo vinavyowadhuru wenzake. Jinsi anavyochagua kusikia na kuitikia "sauti" kadhaa zinazopigana na zinazopingana, kila moja ikiwania ukuu, humkuza kuwa alivyo na kuumba vile atakavyokuwa yeye mwenyewe na wenzake kama jamii kwa pamoja. Kila mshiriki wa shairi hili katika mchakato mzima huchunguza mawazo na maisha ya mshiriki mwenzake na kujenga hali mseto ya tanzia-ramsa (Bressler, 2007:46). Hii ndiyo falsafa ya Abdalla kuhusu kusitisha dhuluma na ukatili, kwamba majadiliano baina ya mtu na nafsi yake ni jambo lisiloepukika.

### **Kujenga Taswira Kamili: Si Kurekodi Tu, Nakualika Tubadili Mambo**

Ushairi umekuwa rekodi muhimu ambayo imeishia kuhadithia kisa kisichosimulika. Kudumu kwake kunatokana na mbinu ya washairi kuepuka lugha ya moja kwa moja ya matukio ya kuogofya ambayo inaweza kuubadili hadi kuwa sanaa ya kuogofya. Ni wazi kwamba, ushairi unaweza kuwasilisha machafuko na maovu halisi kwa ubatini na usahihi usiowezekana ikiwa mbinu na tanzu nyinginezo zingetumika.

Mashairi hutumiwa kama rekodi ya kutuhimiza kushuhudia vurugu na ukatili. Picha zinazotumiwa zinajumuishwa na hisia za ndani kuibua dhana kwamba chochote kinachoandikwa huwa zaidi ya kile tunachoweza kuelewa. Yaani, mashairi huwa nje ya uzoevu wetu wa kawaida, hata wakati ambao msomaji anaalikwa kushuhudia kile kinachowasilishwa. Hili linatuhimiza kusoma na kuziba mapengo. Katika hali hii, mshairi ana uwezo wa kujitenga na shairi, na kuhisi kuwa hashukiwi na kuhusishwa na hali inayoelezwa katika shairi. Huku kumvuta msomaji na kumuingiza katika shairi na kumpa fursa ya kushiriki kulitunga ni dhihirisho kwamba hadhira ni sehemu ya usimulizi. Kwa njia hii, msomaji hushiriki kisaikolojia kwenye eneo la kuogofya la vurugu.

Mvua inaashiria mambo kama vile nguvu ya kurutubisha, ishara ya utakaso, ishara ya kuteseka au bahati mbaya (Cirlot, 2001:271; Ferber 2007:165-166). Mara nyingi, mvua huwa kama kiwakilishi cha hali mbaya ya hewa na hivyo kuwa ishara ya nyakati zozote za kuhuzunisha maishani. Katika shairi la "Telezi" (uk. 24-25) mtunzi anatumia jazanda kwa wingi kujadili jinsi polisi walivyotumia nguvu za kupita kiasi katika wakati wa ufunguzi rasmi wa hospitali ya Nyanza General huko Kisumu ambayo Tume ya Ukweli Haki na Maridhiano inachukulia kama aina ya mauaji yanayovuka haki (TJRC, 2013). Wakati wa ufunguzi wa hospitali ya Jaramogi Oginga Odinga Teaching and Referral machafuko yasiyotarajiwa yalitokea. Inasemekana kuwa polisi walifyeka msitu wa waandamanaji ili kupata barabara ya msafara wa Rais kupita. Kuhusu tukio hili, TJRC vol. IIA inasema,

Odinga hakuwa amelikwa, lakini yeye na wafuasi wake walikuja kwa nguvu wakipiga kelele ‘Dume’ ... Katika ghasia zilizofuata, fujo kamili zilitokea, msafara wa Rais pamoja na kikosi kinachoogopwa cha Jeshi la kukabiliana na fujo [GSU] walimzingira Rais, wakaufyatulia risasi umati uliowatishia na kuendelea hivyo kilomita 25 nje ya mji. [Katika] 'mauaji ya Kisumu' ... wengi walipigwa risasi na ulinzi wa Rais wakafa, wakiwemo wanafunzi wa shule (TJRC, 2013:).

Kufyatuliwa risasi huku ndiko kunarejelewa kama mvua katika ubeti wa kwanza wa shairi “Telezi”. Kulingana na mshairi, mvua ilianguka ikiandamana na ngurumo za radi na mweso. Katika ubeti huu, mshairi anasema:

Mvuwa iliyonyesha, ya maradi na ngurumo  
Kutwa na kucha kukesha, kunyesha pasi kipimo  
Haikuwanufaisha, wenye kazi za vilimo  
Wenye kazi za vilimo, walifikwa na hasara

Athari za mvua yenyewe ambazo zinajumuisha vifo vya wanafunzi kadhaa zimetajwa katika ubeti huu, pale anaposema kwamba mvua iliyonyesha haikuwanufaisha wenye kazi za vilimo. Kwa mantiki hii, mtunzi wa diwani hii analenga kuishawishi akili ya msomaji kwa kumtaka ajisake nafsi yake kutambua mchango wake kwa hali iliyopo. Msomaji anaalikwa kujaza mapengo yaliyoachwa kwenye ushairi huu, kama vile mvua ilinyesha lini na wapi. Jukumu hili la kujaza ambalo mshairi humkabidhi msomaji ndilo husukuma mbele juhudi za makabiliano ili kumaliza mateso na dhuluma katika jamii na kumpa nafasi ya kuelewa utungo kwa undani. Kwa hiyo, ushairi huwaokoa waliodhulumiwa. Kwa mshairi, maisha ni mwito wa kuhakikisha msomaji anasikia kilio cha waathirika katika mchakato wa kujaza mapengo ya lugha dokezi iliyotumiwa. Washairi huibua taswira za kuogofya za mateso ambayo msomaji huziwazia na kuzijenga akilini. Hili huyapa pumzi na nguvu mpya maelezo ya maovu na mateso kwa kutajirishwa na msomaji kujaza mapengo. Kiu ya msomaji inakuwa kichocheo cha kujaza sehemu zinazokosekana. Njia hii inawashirikisha na kuwachochea wasomaji kuchukua hatua.

Washairi hugema kutoka kwenye utata wa lugha kuwasilisha kile ambacho vinginevyo hakiwasilishiki. Hili linafanya ujumbe wao kuvuka vizuizi vya udhibiti na uchunguzi. Inaweza kuonekana kana kwamba tungo za Kiswahili si kile tunachoweza kukiita "mshairi ya uasi mkali." Lakini hili si kweli kwa sababu lugha hii ina utata wa ndani wa maana unaotokana na mwegemeo wake mkubwa kwenye muktadha ili kuelewa maana iliyofichamwa, jinsi inavyodhihirika hapa kupitia matumizi ya neno “mvuwa”.

Katika shairi la "Mamaetu Afrika" (kur. 36-41), mshairi anapiga hatua zaidi kuliko kuweka tu kumbukumbu ya matukio na kuonyesha vyanzo, matokeo na

kupendekeza suluhisho kwa migogoro ya mara kwa mara inayosababisha machafuko nchini Kenya na barani Afrika kwa jumla. Kwa hivyo, mshairi si mhifadhi na mtunzaji tu wa matukio bali ni mwanadamu anayezungumza kwa wanadamu wengine (Bressler, 2007:36). Mama huwakilisha utambuzi wa pamoja (Ferber, 2007). Kwa kutumia ishara hii, mshairi anadokeza kuwa ni muhimu kwa wananchi wote kuwa na umoja ili kutambua adui wao halisi ni nani ndipo wapate suluhisho la kupata suluhisho la kudumu kwa vita vya mara kwa mara. Uhasama kati ya wanajamii ulianzishwa na wakoloni ambao baada ya kutambua kuwa wameshindwa walibadilisha mbinu na mikakati. Kwa hiyo, dhuluma na ukatili wa baadaukoloni ni uzao wa kipindi kilichotangulia. Wameendelea hadi sasa ama kwa mwelekeo au kwa mbinu. Hoja ya kimwelekeo inayakinishwa na ukweli kuwa jamii ilijisalimisha kwa mbinu ya tenga-tawala iliyoletwa na mkoloni (tazama beti 14-16, 31-34). Hoja ya kuendeleza dhuluma kwa mbinu inashikiliwa na ukweli kuwa mbinu zilizotumiwa wakati huo zinaendelea kutumika hadi sasa. Wakati wa ukoloni, jeshi liliwachunguza na kuwahoji watu ili kupata habari kutoka kwao kuhusu Maumau (Kituo cha Sheria, 2013). Dhuluma na mateso yaliibuka kutoka kwenye michakato hii ya uchunguzi iliyoenea na kwa taratibu ikageuzwa kuwa asasi kamili ya utawala. Jeshi hilo liliendelea kutumia mbinu zilezile za ukatili hata katika kipindi cha baada ya uhuru hata katika *Operesheni Okoa Maisha* iliyofanyika Machi 2008 mlimani Elgon. Mshairi anasimulia hali hii ya kusikitisha katika "Mamaetu Afrika"; anaonelea kuwa umoja ni muhimu katika kumaliza hali hii. Katika ubeti wa 13, mshairi anaashiria uovu uliofanywa wakati wa vita vya Maumau vilivyoishia kwenye vifo vya watu kadhaa kama inavyojitokeza katika beti 18 hadi 21. Katika ubeti wa 21 mshairi anasema:

Nyingi mno damu yetu, ikabidi kumwaika  
Baadhi ya ndugu zetu, roho zao zikatoka  
Na kila kilicho chetu, kwa wingi kikatumiwa  
Kwa kutaka kuiweka, hadhi yetu nawe Mama

Mshairi anarejelea damu iliyomwagika katika vita vya Maumau vilivyohusu kupata uhuru. Kwa mujibu wa ripoti ya TJRC Juz. 4 na Juz. IIC, wenyeji na wakoloni walitenda maovu. Kwa hakika, Maumau waliwashambulia wazee, wanawake na watoto walioshukiwa kuwa walifaidi kutoka kwa uongozi wa wakoloni (TJRC Juz. 4 12 na Juz. IIC 93). Katika vita hivi, wengi walipitia vitisho, maovu, ukatili na uhalifu mkubwa. Aidha, katika vita hivi, mauaji ya Lari na Hola yalitokea. Inasemekana kuwa katika mauaji ya Lari, Maumau waliwanyonga watu walioshirikiana na wakoloni. Katika kambi ya Hola wafungwa 11 wa kisiasa waliuawa (TJRC, 2013; Kituo Cha Sheria, 2013). Haya ndiyo yanayoshughulikiwa katika ubeti huu.

## Hitimisho

Kumekuwa na maovu mengi katika historia ya Kenya kuliko inavyoweza kujadiliwa kikamilifu katika makala kama hii. Kwa mshairi, matendo haya ya unyama hufanya kazi ya kuwekeza katika lugha na kuipa jukumu la kuelezea hizo hofu ngumu nusura kutowezekana. Kupata maneno ambayo yanaweza kukabili yale yasiyoweza kusemwa ni shughuli nzito. Hata hivyo, makala hii imejaribu kukita hofu ya maovu kwenye taswira, jazanda, na lugha dokezi ya kitamathali japo zinachopeza uchungu. Mjadala umethibitisha kwamba, vita ambavyo ni chemichemi ya machafuko vimekuwa jambo la kila mara katika safari ndefu ya kusaka uhuru na haki nchini Kenya. Ukweli huu haukuepuka makini ya mtunzi wa *Sauti ya Dhiki*. Mtunzi anachukulia hili kuwa miongoni mwa maovu mabaya zaidi, na kusitishwa kwake kunahitaji subira, muungano na kujitolea kwa wanajamii wote.

## Marejeleo

- Abdalla, A. (1973). *Sauti ya Dhiki*. Nairobi: OUP.
- Boushaba, S. (1988). An Analytical study of some problems of literary translation: a study of two Arabic translations of the Prophet. Phd thesis submitted to The University of Salford.
- Bressler, C. E. (2007). *Literary Criticism: An introduction to theory and practice*. London: Pearson Prentice Hall.
- Chacha, N.C. (1992). *Ushairi wa Abdilatif Sauti wa Utetezi*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.
- Cirlot, J. E. (2001). *Dictionary of Symbols* (2<sup>nd</sup> ed.). London: Routledge.
- Dawes, J. (2007). *That the world may know*. Cambridge: Havard University Press.
- Ferber, M. (2007). *A Dictionary of Literary Symbols*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Karari, P. (2014). Ethnopolitical Violence, Transitional Justice and Peacebuilding in Kenya: Nurturing a Tripartite Hybridity. Phd Thesis submitted to The University of Manitoba.
- Katho, D. (2013). Power-Sharing in Resolving Africa's Electoral Conflict. M.A thesis submitted to the University of Nairobi.
- Kituo cha Sheria. (2013). *Summary of the Truth, Justice and Reconciliation Commission (TJRC) Report*. Nairobi: Kituo cha Sheria.
- Maitaria, J. N. (2015). Sauti ya kiharakati katika ushairi wa Abdilatif Abdalla. In M. Mukuthuria, J. O. Ontieri, M. Kandagor, & L. Sanja (Eds.), *Kiswahili na Maendeleo ya Jamii* (pp. 193 - 210). Dar es Salaam: TATAKI (CHAKAMA).
- Njozi, H. M. (1998). Critical Artistry in *Utenzi wa Shufaka*. AAP, 55, 41-51.

- Povey, J. F. (1993). English-Language Fiction from South Africa. In O. Owomoyela (Ed.), *A history of twentieth century African literatures* (pp. 84 - 104). Nebraska: University of Nebraska Press.
- Samson, R. (1996). Tungo za kujibizana: "Kuambizana ni sifa na kupendana". *AAP*, 47, 1-10.
- TJRC. (2013). *Report of the Truth, Justice and Reconciliation Commission Vols 1 - 4*. Nairobi: Truth Justice and Reconciliation Commission (TJRC), Kenya.
- Treasure, G. (1985). *The Making of Modern Europe (1648 - 1780)*. London: Routledge.
- UNESCO. (2002). *Manual of the General Conference*. Paris: United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization.
- Wambura, A. C. (2008). Effects of 2007 Post Election Violence in Kenya: A case study of Kisumu City. MA Research Project submitted to the University of Nairobi.
- Wamitila, K. W. (2008). *Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide~Muwa.